Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ELIMU Bulletin

JARIDA LA MTANDAONI: Toleo Na.23 - 2022

wizara_elimuTanzania wizara_elimuTz www.facebook/moestvt.com www.wyestu.blogspot.com www.moe.go.tz ELIMUTZ

Tunaendelea kuboresha Elimu yetu

Serikali yakabidhiwa Chuo cha Ufundi Stadi Kagera

- KAZI IENDELEE -

BODI YA UHARIRI

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

Atupele Mwambene
Mkurugenzi wa Sera na Mipango

Sylvia Lupembe
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Nelly Mtema
Mhariri Msaidizi na Mwandishi TSN

Wachangiaji:
Oliva Kato
Elizabeth Pancras
Ipyana Mwaipaja

Mawasiliano:
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Afya - Dodoma
S.L.P. 10, 40479 DODOMA.
Simu: +255 26 296 3533

Jarida hili linatolewa na
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

TAHARIRI

Elimu Ujuzi kichocheo cha maendeleo

Serikali inatoa kipaumbele katika mafunzo ya ufundi stadi kwa kuwa yanawezesha watu kupata ujuzi, maarifa na stadi za kutenda kazi halisi katika fani na kada mbalimbali.

Hivi karibuni Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizungumza na wananchi wa Mkoa wa Kagera baada ya kupokea na kuzindua Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Kagera, alisema kuwa uzalishaji wa watu wenye ujuzi wa kutenda kupitia mafunzo ya ufundi stadi nchini unakwenda sambamba na mahitaji ya nguvukazi katika ulimwengu wa sasa.

Mhe. Rais aliongeza kuwa kila kiwanda, kampuni au shirika linalotoa ajira huhitaji kuajiri watu wenye stadi zinazohitajika ambazo zinaleta thamani na kuongeza ufanisi na tija katika uzalishaji.

Tukizungumzia tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana, ambalo nchi nyingi za Afrika ikiwemo Tanzania zinakumbana nalo, ufundi stadi ni eneo la msingi kabisa katika kuchangia kupunguza tatizo hilo kwani unampa mtu fursa ya kuajiriwa ama kujiajiri mwenyewe.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeshaanza kutekeleza mkakati wa kuwa na Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi katika mikoa na wilaya zote nchini na hili litaongeza fursa za vijana kupata Elimu Ujuzi karibu na maeneo yao.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Adolf Mkenda amekuwa akisikika katika vyombo vya habari akisema kuwa karibu mikoa yote imejengewa Vyuo hivyo huku Vyuo vya mikoa ya Njombe, Geita na Rukwa vikiwa katika hatua mbalimbali za ukamilishaji na Mkoa mpya wa Songwe ukiwa umetengewa fedha ya kuanza ujenzi.

Aidha, anasema katika Mwaka wa fedha 2022/23 Wizara ya Elimu tayari imetenga Shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kuanza ujenzi katika Wilaya 63 ambazo bado hazina vyuo hivyo. Kongole kwa Serikali na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuona umuhimu wa kuwa na vyuo hivyo ambavyo vitasaidia mamia ya vijana kupata ujuzi na maarifa yatakayowawezesha kuwa na stadi za kujiajiri ama kuajiriwa na kupunguza changamoto ya ukosefu wa ajira nchini.

Hima kwa wazazi na walezi kuhakikisha tunawapeleka vijana wetu katika vyuo hivi ili waweze kujipatia ujuzi, maarifa na stadi za kuwawezesha kujitegemea na kuchangia katika uchumi wa Taifa.

Uwekezaji katika Elimu >

Serikali yakabidhiwa Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma Kagera

Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekabidhiwa Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Kagera kilichojengwa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China.

Mradi wa ujenzi wa Chuo hicho umegharimu jumla ya Dola za Kimarekani 9,552,380 sawa na fedha za Kitanzania Shilingi bilioni 22, gharama ambayo inajumuisha ujenzi wa miundombinu ya majengo na mifumo ya maji safi na taka na uwekwaji wa baadhi ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia, mashine na samani katika majengo.

Chuo hicho ambacho kilikabidhiwa kwa Serikali na kuzinduliwa rasmi na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivi karibuni ambapo katika hafla ya makabidhiano hayo ameishukuru Serikali ya China kwa kuwa imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali ya kusaidia kuboresha elimu na kuendeleza ujuzi nchini.

"Msaada huu umesaidia kwa kiasi kikubwa katika kuzalisha nguvukazi yenye ujuzi na mahiri kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Kwa hakika, China inaendelea kuonesha kuwa ni rafiki wa kweli, wa karibu na mdau wa kutegemewa katika maendeleo ya nchi yetu," amesema Mhe. Rais.

Aidha, Rais Samia amesema ili kuhakikisha wazazi na walezi wa Mkoa wa Kagera wanapeleka vijana wao katika chuo hicho kupata ujuzi, Serikali itakuwa ikitoa zaidi ya bilioni moja kila mwaka kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Chuo hicho na kuwezesha wazazi na walezi kulipia ada kidogo ambayo wataimudu.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda akizungumza katika hafla hiyo amesema Chuo hicho cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Kagera ni hatua nyingine muhimu katika mpango wa Serikali kupitia Wizara ya Elimu wa kukamilisha ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya ngazi ya Mikoa.

Ameongeza kuwa kwa sasa, mikoa

Inaendelea uk 4

Uwekezaji katika Elimu >

Serikali yakabidhiwa Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma Kagera

Inatoka uk 3

mingine ambayo ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Mikoa unaendelea ni Njombe, Simiyu, Rukwa na Geita na mpango wa ujenzi wa Chuo cha Mkoa wa Songwe unaendelea kukamilishwa ili ujenzi uanze na kwamba tayari fedha za kuanza ujenzi zilishatengwa.

Naye Balozi wa China nchini, Mhe. Chen Mingjian amempongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa mikakati mbalimbali aliyoifanya ya kubadilisha na kuboresha mfumo wa elimu na mazingira ya kufundishia na kujifunzia ikiwemo kuwekeza katika Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

Mhe. Mingjian ameongeza kuwa mikakati hiyo imewezesha kutoa fursa kwa makundi maalum kupata elimu bila changamoto. Aidha, amepongeza mchakato wa mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na mabadiliko ya mitaala yanayolenga kuboresha elimu nchini.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii Mhe. Stanslaus Nyongo ameipongeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kutekeleza kwa kasi mchakato shirikishi wa mapitio ya Sera na Mabadiliko ya Mitaala yanayolenga kutoa elimu ujuzi.

Chuo hicho ambacho kitatoa programu tisa za Ufundi Stadi na Huduma kina majengo ya karakana, madarasa, ukumbi wa mihadhara, maabara ya kompyuta, chumba cha maktaba, ofisi za walimu, jengo la utawala linalojumuisha ofisi mbalimbali pamoja na nyumba mbili za walimu zenye kuchukua familia nne.

Majengo mengine ni mabweni mawili ya wanafunzi, jiko na bwalo la chakula pamoja na miundombinu wezeshi ikihusisha uzio, usawazishaji ardhi kwa ajili ya viwanja vya michezo, barabara za ndani, maeneo ya maegesho, taa za barabarani na mitaro ya kusafirisha maji ya mvua.

Mafunzo umahiri wa bidhaa >

Serikali yaimarisha Mafunzo ya Umahiri wa bidhaa za ngozi nchini

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Mradi wa Kujenga Ujuzi kwa Maendeleo na Uingiliano wa Kikanda katika Afrika Mashariki (EASTRIP) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia inaendelea na utekelezaji wa ujenzi wa Kituo cha Umahiri katika sekta ndogo ya ngozi.

Kituo hicho kinachojengwa katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) kampasi ya Mwanza kinalenga kuimarisha mafunzo ya ujuzi juu ya bidhaa za ngozi yanayotolewa katika kampasi hiyo.

Akielezea namna wizara ilivyojipanga katika kukiimarisha kituo hicho mara baada ya kukagua utekelezaji wa mradi huo, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema Shilingi bilioni 19.6 zimetengwa katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/23 kwa ajili ya kituo hicho.

"Fedha hizo zinatumika katika kufanya ukarabati na kuongeza miundombinu ya kufundishia na kujifunzia kwa lengo la kuhakikisha mafunzo yanayotolewa yanatoa ujuzi ili kuongeza wataalamu katika teknolojia ya ngozi nchini watakaoleta tija katika mnyororo wa kuongeza thamani mazao ya ngozi," amesema Prof. Mkenda.

Prof. Mkenda amesema Serikali itahakikisha DIT inakuwa kituo cha umahiri cha utoaji mafunzo ya ufundi na ujuzi katika kuchakata mazao ya ngozi na utengenezaji bidhaa mbalimbali za mazao hayo.

Kiongozi huyo ameongeza kuwa mafunzo hayo yanatolewa katika Kanda ya Ziwa kwa kuwa kuna malighafi ya kutosha ya ngozi, hivyo anatarajia kuona chuo hicho kinanufaisha vijana wengi ili wakimaliza mafunzo hayo waweze kuwa mahiri na kujiariri ama kutoa ajira.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala akizungumza katika ziara hiyo ameipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuboresha miundombinu ya elimu katika Mkoa wa Mwanza ikiwemo kampasi ya DIT ambayo itatoa mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi kupitia mazao ya ngozi.

Awali akitoa taarifa ya Chuo, Mwenyekiti wa Baraza la DIT Mhandisi Dkt. Richard Masika amesema, DIT imekuwa ikitoa mafunzo ya ufundi wa utengenezaji bidhaa za ngozi kwa nadharia na vitendo kwa kuwajengea uwezo vijana ili waweze kushindana katika soko la ajira kitaifa na kimatafa.

Uwezeshaji Elimu>

Maafisa Elimu ya Watu Wazima kuwezeshwa kutekeleza majukumu yao

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Omari Kipanga ametoa wito kwa Wakurugenzi wa Halmashauri kutenga bajeti kwa ajili ya kuwawezesha Maafisa wanaosimamia Elimu ya Watu Wazima kuwafikia walengwa kwa urahisi.

Mhe. Kipanga ametoa wito huo wakati akifunga maadhimisho ya Wiki ya Elimu ya Watu Wazima yaliyofanyika katika Viwanja vya DUCE Jijini Dar es Salaam ambapo amesema kwa kufanya hivyo itawezesha utekelezaji wa shughuli za Elimu ya Watu Wazima katika eneo husika kwa ufanisi.

Amesema katika kuipa uhai Elimu ya Watu Wazima pamoja na kutengewa bajeti, Maafisa Elimu ndani ya Mikoa na Halmashauri wanapaswa kuhakikisha wanahamasisha, kuanzisha, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa programu mbalimbali za Elimu ya Watu Wazima.

"Niwasihi Maafisa Elimu ya Watu Wazima pamoja na kusimamia kazi katika maeneo yenu shirikianeni na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kuendeleza jitihada za kuhakikisha kuwa madarasa ya MEMKWA yanasimamiwa na kuwa na vitendea kazi vinavyokidhi mahitaji ya ufundishaji na ujifunzaji," amesema Mhe. Kipanga.

Akizungumzia mapitio ya Sera na Mitaala yanayoendelea, Mhe. Kipanga amesema wizara bado inapokea maoni ya wadau kuhusu maboresho hayo huku ikiendelea na uchambuzi wa maoni ambayo yamepokelewa ili kukamilisha kazi hiyo.

Aidha amesema lengo la Serikali ni kuhakikisha kila mtoto wa Kitanzania anapata fursa ya kupata elimu iliyo bora ndio maana imeweka Sera ya Elimu bila ada kuanzia Elimu ya Awali hadi Kidato cha Sita huku ikiwarudisha shule wanafunzi waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali waweze kuendelea na masomo ili watimize ndoto zao.

Akimwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu katika kilele hicho Kamishna wa Elimu, Dkt. Lyabwene Mtahabwa amesema katika kukabiliana na changamoto ya idadi ya watu wasiojua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu, Wizara inatekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kisomo cha Elimu kwa Umma ambao unalenga kuboresha programu za kisomo na elimu kwa njia mbadala. Pia imeandaa "National Qualification Framework" mfumo ambao kwa mara ya kwanza umetambua programu za Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi.

Maonesho ya Maadhimisho ya wiki ya Elimu ya Watu Wazima yaliyofanyika Jijini Dar es Salam kuanzia Oktoba 17-21, 2022 yalikuwa na kaulimbiu isemayo "Kuboresha mazingira ya kujifunza kusoma na kuandika yatakayozingatia ubora, usawa na ujumuishi wa makundi yote" na yameshirikisha Vyuo Vikuu, Taasisi zilizo chini ya Wizara, Maafisa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi Wilaya na Mikoa yote Tanzania Bara, Mashirika ya Kimataifa pamoja na wadau mbalimbali wanaojishughulisha na utoaji wa Elimu ya Watu wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi hapa nchini.

Maadhimisho Vyuo Vikuu >

Miaka 60 ya Chuo Kikuu DSM na 17 ya DUCE: Vyuo Vikuu vyahimizwa kufanya tafiti

Vyuo Vikuu nchini vimetakiwa kufanya tafiti, zikiwemo tafiti kuhusu namna ambavyo elimu ya juu itakidhi matakwa ya sasa ya jamii ya Kitanzania.

Agizo hilo limetolewa jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Francis Michael wakati wa Kongamano la Maadhimisho ya Miaka 60 ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Miaka 17 ya Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE).

Amesema ni vizuri kufanya utafiti wa kina kuhusu mwelekeo wa sasa wa kitaifa na kimataifa kisha kutafakari ni namna gani vyuo vyetu vitawawezesha wahitimu kuendana na mwelekeo huo.

"Kama mnavyofahamu, kumekuwa na mjadala kuhusu uwezo wa kujiajiri miongoni mwa wahitimu wa vyuo vikuu, mjadala ambao kwa namna moja au nyingine umezua maswali kuhusu mitaala ya elimu nchini. Kutokana na mjadala huu, Rais Samia Suluhu Hassan alizungumzia umuhimu wa kuipitia upya mitaala ili iendane na matakwa ya ulimwengu wa sasa, ikiwemo uwezo wa wahitimu kujiajiri na kuwa wabunifu, hivyo ni muhimu kutafakari ni kwa namna gani DUCE na vyuo vingine vinachangia katika jitihada hizi,"amesema Dkt. Michael

Aidha, amesema kama ilivyo kwenye vyuo vingine, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itaendelea kutoa ushirikiano kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, na Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam katika dhamira yake ya kuendelea kutoa walimu bora, ambao wanahitajika ili kufikia lengo la kutoa elimu bora kwa Watanzania wote.

Kwa upande wake, Rasi wa Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Prof. Stephen Maluka amesema Chuo hicho katika kipindi cha miaka 17 tangu kuanzishwa kwake kimepata mafanikio makubwa. Akitaja baadhi ya mafanikio hayo kuwa ni pamoja na kuongezeka kwa wahitimu kutoka 522 Mwaka 2008 hadi kufikia 16,330 Mwaka 2021, programu kutoka Shahada za awali Nne hadi Tano.

Prof. Maluka ameishukuru Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kukisaidia Chuo kusomesha watumishi, ujenzi na upanuzi wa miundombinu kupitia miradi yake mbalimbali hivyo kutatua changamoto ya miundombinu katika chuo hicho hivyo kupunguza gharama za kusomesha watumishi hadi kufikia ngazi ya Shahada ya Uzamivu.

Aidha, ameishukuru Serikali, kwa kukiletea Chuo hicho Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (Higher Education for Economic Transformation – HEET Project) kwani wameweza kusomesha watumishi wanataaluma katika vyuo maarufu duniani katika ngazi ya Umahiri na Uzamivu.

Pia, kupitia mradi huo, Chuo kinatarajia kutumia zaidi ya Dola za Kimarekani 4,357,827.61 ambazo ni sawa na takribani Shilingi bilioni kumi za Kitanzania kwa ajili ya kuendelea kufanya ukarabati wa miundombinu na kujenga majengo na miundombinu mingine mipya.

Maadhimisho ya Miaka 60 ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Miaka 17 ya Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam yamepambwa na maonesho ya kazi mbalimbali za utafiti na uvumbuzi zilizofanywa na wanataaluma wa chuo hicho.

Pongezi kwa WyEST >

Kamati ya Bunge yapongeza mfumo wa kielekroniki wa usahihishaji mitihani ya Taifa

Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii imepongeza Wizara ya Elimu na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) kwa kuwa na mfumo wa kielektroniki wa usahihishaji mitihani ambao umerahisisha zoezi la usahihishaji mitihani ya Taifa.

Pongezi hizo zimetolewa hivi karibuni na Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Stanslaus Nyongo wakati Kamati ilipofanya ziara katika Taasisi hiyo ambapo mfumo huo kwa sasa unatumika kusahihisha mitihani ya darasa la Saba na Ualimu.

Kamati hiyo pia imeishauri Wizara kuwatambua kitaifa Watanzania waliovumbua mfumo huo kutokana na kuwa umejibu changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na kufupisha muda wa usahihishaji.

"Huu uvumbuzi unatakiwa ulindwe na muone namna bora ya kuwatambua Kitaifa wavumbuzi wa mfumo huu pamoja na kuubiasharisha kwani Watanzania wengi wana imani kubwa na utendaji kazi wake uliofanikiwa kupunguza malalamiko kwa kiasi kikubwa," amesema Mhe. Nyongo.

Kamati hiyo imetoa maoni na mapendekezo ya kuimarisha utendaji ikiwemo kuwezesha upatikanaji wa vifaa vya kutosha vitakavyowezesha mfumo huo kutumika Kikanda ili kurahisisha zaidi zoezi la usahihishaji mitihani.

Akiongea kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Omari Kipanga (Mb) ameishukuru Kamati hiyo kwa kutembelea NECTA na kuahidi kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hiyo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya NECTA, Prof. William Anangisye amesema kuwa kwa sasa wataalamu wanaendelea kuandaa mifumo kwa ajili ya usahihishaji wa mitihani ya Darasa la Nne na ile ya Sekondari.

Chakula na Lishe Shuleni >

Kipanga: Utoaji wa chakula na lishe shuleni huchangia maendeleo kitaaluma kwa mwanafunzi

Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Omari Kipanga (Mb) amesema utoaji wa chakula na lishe kwa wanafunzi wakiwa shule ni suala muhimu kwa kuwa upo uhusiano mkubwa kati ya afya ya mwanafunzi na maendeleo yake kitaaluma.

Mhe. Kipanga amesema hayo jijini Dodoma katika hafla ya utiaji saini kujiunga na Muungano wa Chakula Shuleni ambapo amesema mwanafunzi anapokosa chakula shuleni hukosa usikivu wakati wa ujifunzaji, mahudhurio hafifu, utoro wa rejareja na hata kukatisha masomo.

Ameongeza kuwa pamoja na jitihada za Serikali katika kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, upatikanaji wa matokeo mazuri ya elimu hutegemea afya aliyonayo mwanafunzi.

"Mwezi Oktoba, 2021 Wizara yangu ilizindua Mwongozo wa Kitaifa wa Utoaji wa Huduma ya Chakula na Lishe kwa Wanafunzi wa Elimumsingi ili kuweka utaratibu wa kitaifa ambao utawezesha wanafunzi kupata huduma hiyo muhimu. Naishuruku OR-TAMISEMI kwa kuendelea kusimamia utekelezaji wa mwongozo huu katika Mikoa na Halmashauri zote nchini," amesema Mhe. Kipanga.

Akizungumzia kujiunga na Muungano wa Chakula Shuleni amesema Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetia saini fomu ya kujiunga na muungano huo, ikiwa lengo ni kumwezesha kila mwanafunzi kupata lishe bora, afya na elimu.

Aliongeza kuwa pamoja na kuwezesha wanafunzi kupata lishe shuleni, muungano huo utatuwezesha kupata uzoefu wa namna nzuri ya kutekeleza mpango wa chakula shuleni kwa kushirikisha jamii kwani muungano huo ni kundi la kimataifa linalojumuisha nchi mbalimbali duniani, mashirika ya kiraia, wasomi na sekta binafsi.

"Kujiunga na muungano huu kutawezesha wadau wetu wa maendeleo, mashirika yasiyo ya kiserikali, kampuni binafsi pamoja na vyombo vya habari, kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa chakula na lishe shuleni," amesema Mhe. Kipanga.

Ametaja nchi za Afrika ambazo tayari zipo kwenye muungano huo kuwa ni Angola, Benin, Burkina Faso, Burundi, Kameruni, Chad, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Misri, Ethiopia, Gambia, Guinea, Kenya, Lesotho, Liberia, Madagasca, Mali, Maurtania, Morocco, Msumbiji, Namibia, Niger, Jamhuri ya Kongo, Rwanda, Senegal, Somalia na Sudan.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani Sarah Gordon-Gibson ameipongeza Serikali ya Tanzania kwa kujiunga na Muungano wa Chakula Shuleni kwani kwa kufanya hivyo ni kuwekeza kwa watoto wetu ambao ndio taifa la kesho.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Suzan Nusu amesema tukio la kutia saini kujiunga na Muungano wa Chakula Shuleni limeonesha dhamira ya dhati ya Serikali kuhakiksha watoto wote wanapata chakula shuleni na kwamba wanaahidi kusimamia utekelezaji wake ili watoto wasome bila changamoto zozote.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wanafunzi mbalimbali wa shule za Msingi na Sekondari mkoani Dodoma ambao wameshiriki katika hafla hiyo wameipongeza Serikali kwa kujiunga na muungano wa Chakula Shuleni kwani utawawezesha kupata chakula shuleni na kuwaepusha na vishawishi vinavyoweza kukatisha ndoto zao za kupata elimu.

Uboreshaji Elimu ya Ualimu >

Serikali yaendelea kuboresha utoaji wa Elimu ya Ualimu

Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeendelea na mikakati ya kuboresha mazingira ya utoaji wa Elimu ya Ualimu kwa kujenga, kukarabati miundombinu na kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Mikakati hii inalenga kuhakikisha mazingira ya utoaji wa elimu hiyo inawezesha kutoa walimu wenye mbinu na uwezo wa kuwaandaa vijana wenye ujuzi na stadi zitakazowasaidia kuingia kwenye soko la ajira kwa kujiajiri au kuajiriwa.

Chuo cha Ualimu Kabanga kilichopo Mkoani Kigoma wilayani Kasulu kimefanyiwa maboresho makubwa kwa kujengewa majengo mapya ambayo yalizinduliwa hivi karibuni na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Rais Samia Mwezi Oktoba, 2022 akiwa ziarani Wilayani Kasulu, Mkoani Kigoma alifungua rasmi matumizi ya majengo hayo yaliyojengwa na Serikali kupitia Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Ualimu (TESP) unaoratibiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Akizungumza na wananchi wa Kasulu, Rais Samia amesema Serikali imeamua kujenga upya Chuo hicho ili kitumike kuandaa walimu ambao watakwenda kufundisha katika shule ambazo zinaendelea kujengwa nchini.

"Leo nimefungua majengo mapya ya Chuo cha Ualimu Kabanga, chuo kikubwa kilichojengwa kwa ushirikiano na ndugu zetu wa Canada na chuo ambacho Waziri wa Elimu amekielezea kuwa ni chuo cha kisasa ambacho kinakwenda kuandaa walimu wengi na bora wa fani zote," amesema Rais Samia

Kwa upande wake, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Adolf Mkenda amesema ujenzi wa majengo hayo mapya umekiwezesha chuo hicho kuongeza uwezo wa kudahili wanafunzi kutoka 400 hadi 800.

Prof. Mkenda amewataka wana Kigoma hasa wa Wilayani Kasulu kuhakikisha wanatumia fursa ya uwepo wa chuo hicho pamoja na Vyuo vya VETA vya Wilaya kwa ajili ya vijana wao kupata mafunzo yatakayowawezesha kujenga ujuzi na umahiri.

Mwalimu tarajali wa mwaka wa pili, Ester Michael ameishukuru Serikali kwa kujenga miundombonu ya chuo hicho kwani imetatua changamoto mbalimbali zilizokuwa zikitokana na miundombinu chakavu ya majengo ya awali.

Chuo cha Ualimu Kabanga kilijengwa upya baada ya majengo ya awali kuwa yamechakaa.

Utekelezaji Elimu Jumuishi>

Wadau watathmini utekelezaji wa Mkakati wa Elimu Jumuishi

Wadau wa Elimu Maalum wamekutana kufanya tathimini ya utekelezaji wa Mkakati wa Tatu wa Taifa wa Elimu Jumuishi ili kubaini changamoto za utekelezaji na kutafuta muafaka ili kuendelea kutoa huduma na elimu bora kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Akifungua kikao cha wadau hao jijini Dodoma, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Francis Michael amewataka wadau hao kuendelea kuchangia juhudi za Serikali katika kuwapatia huduma stahiki wanafunzi wenye mahitaji maalum ili waweze kujifunza bila changamoto na kutimiza ndoto zao.

Dkt. Michael amewataka wadau hao kuweka kipaumbele katika ubore-shaji wa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji hususani kwenye shule, vyuo vya ualimu, vyuo vya maendeleo ya wananchi, vyuo vya ufundi stadi na vi-kuu.

"Tutaendelea kushirikiana nanyi wadau wa elimu jumuishi kuhakiki-sha upatikanaji wa elimu bora kwa wote kwa kuzingatia ujumuishi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Tuweke kipaumbele katika mazingira yao ya kujifunzia na kufundishia ka-tika ngazi zote za elimu," amesema Dkt. Michael.

Aidha, Katibu Mkuu huyo ametaja baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika Serikali ya Awamu ya Sita kuwa ni ujenzi na ukarabati wa miundom-binu rafiki na fikivu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, kununua na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia, vifaa saidizi vya kisasa pamoja na kuandaa kamusi ya lugha ya alama ya Tanzania kwa lengo la kurahisisha mawasiliano wakati wa ufundishaji na ujifunzaji kwa wana-funzi viziwi.

Naye Mkurugenzi wa Elimu Maalum kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Magreth Matonya amesema lengo la kikao hicho ni kufanya tathmini ya pamoja na wadau ya utekelezaji wa mwaka mmoja wa Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi wa 2021/22 – 23/26 ambao umezingatia utoaji wa elimu jumuishi katika ngazi zote za elimu

Ameongeza kuwa kupitia kikao hicho wadau watapata fursa ya kutoa maoni juu ya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na maba-diliko ya mitaala ili kundi hilo lihusish-we ndani yake.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Sense International, Naomi Lugoe ameishukuru Serikali kwa kushirikisha taasisi na mashirika yanayohudumia watoto wenye mahitaji maaalum kuhakikisha wanapata elimu bila changamoto yoyote, huku akiwata-ka wazazi kuwapeleka shule watoto wenye mahitaji maalum kwani Seri-kali imeweka miundombinu rafiki na fikivu.

NUKUU >

TUTAJIELEKEZA KATIKA KUFANYA MAPITIO YA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MWAKA 2014 NA KUFANYA MAREKEBISHO KWENYE MITAALA ILIYOPO ILI IELEKEZWE KWENYE KUTOA ELIMU UJUZI KULINGANA NA MAZINGIRA YA NCHI NA SOKO LA AJIRA ,

– Mhe. Samia Suluhu Hassan,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Bungeni - April, 2021

Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

Katibu Mtendaji,
Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 6562,
7 Mtaa wa Magogoni,
11479 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2113694, 2113691
Barua Pepe: es@tcu.go.tz

Mkurugenzi Mtendaji,
Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB),
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo -TAZARA,
Barabara ya Mandela,
P.O. Box 76068,
15471 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 736 665 533/ 739 665 533
Baruapepe: ed@heslb.go.tz

Katibu mtendaji,
Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),
Eneo la Viwanda Mikocheni,
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2624 au 32019,
14112 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2700493-6/9 na 22 2772423
Barua Pepe: esnecta@necta.go.tz

Mtendaji Mkuu,
Baraza la Taifala Elimu ya Ufundi (NACTE),
S.L.P 7109, DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@nacte.go.tz

Mtendaji Mkuu,
Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM),
Nunge Street, Old Catholic Church Road,
S.L.P 71, BAGAMOYO, PWANI.
Simu: +255 23 244 0216
Barua Pepe: adem@adem.ac.tz

Mkurugenzi Mkuu,
Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH),
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P. 4302,
14113 Kijitonyama,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 (022) 2771358/ 2774023/ 2700749
Baruapepe: dg@costech.or.tz

Mkurugenzi Mkuu,
Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),
Plot 132, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 0735 041168
Barua Pepe: director.general@tie.go.tz

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),
S.L.P 34578,
Mikocheni B, Bima Road,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@tea.or.tz
dg@tea.or.tz

Mkurugenzi Mkuu
VETA Makao Makuu,
Plot No. 18, Central Business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
26 DODOMA.
Simu: +255 26 2963661
Baruapepe: info@veta.go.tz

Mtendaji Mkuu,
Tume ya nguvu za Atomic Tanzania (TAEC)
S.L.P 743,
23114 Engutoto, Block J, Plot No 216,
ARUSHA
Simu: +255 272 9700054
Barua Pepe:dg@taec.go.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani,
S.L.P. 35091, Mtaa wa Chuo Kikuu
16103 Dar es Salaam
Simu: +255222410700
Baruapepe: vc@udsm.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
Ardhi University (ARU),
Plot No. 3, Observation Hill Blok L,
University Road,
P.O. Box 35176, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 738 357 310-12
Baruapepe: aru@aru.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili (MUHAS),
9 Barabara ya Umoja wa Mataifa,
Upanga Magharibi,
S.L.P. 65001,
11103 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2150302-6
Baruapepe: vc@muhas.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA),
S.L.P 3000,
Barabara ya Edward Moringe, Mtaa wa Kilimo,
01 MOROGORO
Simu: +255 23 260511-4
Barua Pepe: sua@sua.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
Chuo Kikuu Mzumbe (MU),
S.L.P 1, MOROGORO
Simu:
Barua Pepe: mu@mzumbe.ac.tz
info@mzumbe.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),
S.L.P 259,
Mtaa wa Benjamin Mkapa,
Jengo la Benjamin Mkapa,
41107 DODOMA.
Simu: +255 26 2310001/2/3
Barua Pepe: vc@udom.ac.tz
relations@udom.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),
S.L.P. 23409,
14110 Open University Road,
Kinondoni Municipality,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2668820/ 2668992
Baruapepe: vc@out.ac.tz

RASI wa Chuo,
Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),
Taifa Road Next to Benjamin Willium,
S.L.P 2329,
15105 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2850975
Barua Pepe: principal@duce.ac.tz
dpacademic@duce.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Ushirika Moshi,
06 Barabara ya Sokoine Moshi,
S.L.P 474
KILIMANJARO
Simu: +255 272 751 833
Barua Pepe: info@mocu.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
Chuo Kushiriki Cha Elimu Mkwawa (MUCE),
Mtaa wa Mkwawa Chuo,
S.L.P. 2513,
51111 IRINGA CBD.
Simu: +255 26 2702 751
Baruapepe: principal@muce.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),
S.L.P. 131,
Barabara ya 01 MUST,
01 MBEYA.
Simu: +255(0)25 2957542/4
Barua pepe: vc@mustnet.

Makamu Mkuu wa Chuo,
Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMIST),
Kampasi ya Tengeru, Barabara ya Nelson Mandela,
S.L.P. 447,
23301 TENGERU, ARUSHA
Simu +255 272970001
Baruapepe: vc@nm-aist.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere,
S.L.P 976, Butiama, MARA
Simu:
Barua Pepe: info@mjnuat.ac.tz

Mkurugenzi
Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB),
27 Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,
S.L.P 9283
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2150048/9
Barua Pepe: info@tlsb.go.tz

Katibu Mtendaji,
Tume ya Taifa ya UNESCO,
7 Magogoni Street,
P. O. Box 20384,
11479 DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2126598/ 22 2134292
Baruapepe: info@natcom.go.tz

Mkurugenzi,
Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)
23 Mtaa wa Bibi Titi Mohammed,
S.L.P. 20679,
11103 DAR ES SALAAM
Simu:
Baruapepe: info@iae.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Ufundi Arusha (ATC),
Junction of Moshi-Arusha and Nairobi Roads,
P.O. Box 296,
23105 ARUSHA.
Simu: +255 (0) 27-297 0056
Baruapepe: rector@atc.ac.tz/pro@atc.ac.tz

Mkurugenzi,
Kituo cha Maendeleo Dakawa,
S.L.P 1733,
MOROGORO.

Mkuu wa Chuo,
Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),
Kona ya Bibi Titi na Barabara ya Morogoro
S.L.P 2958
11104 DAR ES SALAAM
Simu:
Barua Pepe: principal@dit.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA),
30 Barabara ya Kibada,
S.L.P 9193,
17107 Kigamboni,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Baruapepe: rector@mnma.ac.tz